*Mulika, Na. 41 (2), 162-174*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Dhima ya Methali Kinzani

*Joseph Nyehita Maitaria*[1]
Chuo Kikuu cha Karatina

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.3

**Ikisiri**

Maadili katika jamii ni kipengele muhimu cha utamaduni na aghalabu huwasilishwa kupitia methali. Kimsingi, methali ni kauli za kifalsafa zinazotumiwa kuelezea na kuelekezea masuala kuhusu maisha ya wanajamii. Watu wanapozungumza, methali hujitokeza kama matini za ndani kwa ndani. Hivyo, methali hubeba ujumbe wa jumla unaohitaji kupatanishwa na miktadha ya kijamii. Mazingira haya huakisi mtazamo na tajiriba za jamii. Methali zinapotumiwa, huwa kurunzi ya kuukoleza zaidi ujumbe. Zinapotumika katika mazungumzo, matarajio ni kuibua jibu au tendo; kuonya kwa kuzingatia utamaduni wa jamii; kusuta matendo na kukemea matendo hasi ya watu. Katika uelekezaji wa maadili katika jamii, methali hutoa maelezo au kusuta kwa kuzingatia misimamo 'mikali'. Methali hizo zimekuwa zikichukuliwa kwa ujumla kuwa zinapingana na zina mwelekeo hasi. Makala haya yanahakiki dhima ya methali kinzani katika kubainishia zaidi ujumbe wa kimaadili. Aidha, inabainishwa kuwa, methali zaidi ya moja zinaweza kutumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe wa jumla na uelekezaji wa maadili katika jamii. Methali kinzani ni msingi katika kujengea mazingira ya uwajibikaji binafsi au wa kikundi cha watu.

## 1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha nyingine, ina kauli teule za kifalsafa zinazotumika katika ufunzaji, uelezaji na uelekezaji wa maadili katika jamii. Miongoni mwa kauli hizo ni methali. Aghalabu, kuna jitihada mbalimbali ambazo zimefanywa katika ukusanyaji na uhifadhi wa methali za Kiswahili. Kwa kuzipitia hifadhi hizo; inabainika kuwa, zina miundo inayotofautiana na maana zake zinaweza kufanana au kukinzana (Nsookwa, 2011). Kwa ujumla, methali zimejaa maadili yanayolenga kumsaidia, kumwongoza, au kumwelekeza mwanadamu kwenye misingi bora kwa kuzingatia masuto au mawaidha (Mlacha, 1985; Maitaria, 2019). Huo ni mwelekeo unaojiegemeza zaidi katika makundi ya methali ambazo zinachangiana katika visawe vya maudhui chanya (suluhu sahihi katika kushughulikia masuala changamano). Aidha, dhima za methali zinaweza kuainishwa zaidi kimakundi kwa kuzingatia namna ya uelekezaji na usisitizaji unaozingatia pande mbili za ujumbe zinazowasilishwa (Wafula, 1994). Kama ambavyo methali ni zao la jamii, maana zake hutokana na utamaduni husika.

[1] **Baruapepe:** jmaitaria@karu.ac.ke

## 2.0 Methali katika Kunasihi na Kushauri Wanajamii Kuhusu Maisha

Kimsingi, methali hutekeleza majukumu ya kuwanasihi na kuwashauri wanajamii kuhusu maisha. Kwa maana hii, methali zimesheheni busara na hekima zinazotumika kuyaratili kwa kuyatafakari masuala muhimu kuhusu maisha ya wanajamii (Finnegan, 1970; Madumulla, 1995). Hivyo, methali ni kiunzi cha kuhifadhi na kuendeleza maono na matarajio ya jamii (Maitaria, 2018). Aghalabu, lengo la matumizi ya methali kinzani ni kuwasilisha masuala ya maadili yanayojiegemeza katika utamaduni wa jamii. Hivyo, methali hizo ni kichocheo cha mawazo ili kufikia suluhu au maamuzi mwafaka. Kwa kuzingatia methali, wanajamii huelekezana ili kutoa tahadhari, suluhu na usawazishaji unaohusu vitendo vya watu (Gesero, 2009; Nyariki, 2014). Uelekezaji huo ni wa aina tatu: wa kimaelezo na kurai (methali: '*pole pole ndio mwendo'*, *'haraka haraka haina baraka'* na *'vita havina macho'*); wa maswali ya balagha (methali: '*umejigeuza chachandu kujipalia makaa?'* na *'angurumapo simba mcheza ni nani?'*), na wa ukemeaji au ukaripiaji (methali: *'akutendae mtende, mche asiyekutenda'* na *'mtoto akilia wembe mpe, ukimkata atajifunza'*). Kadhalika, masuala muhimu ya kimaadili huelezwa kwa kauli zenye sifa zinazokaribiana kiufasili kwa kiasi fulani (sifa za kawaida - methali: *'mumewe mama ni baba', 'mkewe baba ni mama'* au ' *mama wa kambo si mama' na 'baba wa kambo si baba'*) au kutofautiana kidogo (sifa isiyo ya kawaida sana - methali: *'mvumilivu hula mbivu'* na '*subira huvuta heri'*). Hivyo, methali hutumiwa kama kioo cha utamaduni wa watu na kama chombo cha kuibulia na kuhifadhi falsafa na busara inayojikita katika tajiriba ya jamii (Wafula, 1994). Katika mazungumzo muhimu, methali hujitokeza kama matini ndani ya matini.

Kwa misingi hii, methali ni kauli zinazobeba ujumbe wa kijumla unaoweza kupatanishwa na miktadha mahususi ya kijamii inayorejelewa katika maingiliano ya mawasiliano ya watu. Hivyo, ni kauli za kumuktadhishwa, na mwafaka huo unapozingatiwa; methali huweza kuwa vivutio vya kuukoleza zaidi ujumbe unaowasilishwa. Katika uwasilishaji wa ujumbe, methali hubainisha hali ilivyo na matarajio yanayostahili kutekelezwa (hatua zinazotarajiwa ni za hiari). Aidha, methali hizo hutumiwa kama kauli zinazotolewa kwa matarajio ya jibu mahususi (hasa kwa kuzingatia tahadhari ya maelezo katika sehemu ya awali katika methali). Kadhalika, methali hizo huonya kuhusu matendo yanayokiuka matarajio ya jamii kwa kusuta na kukemea matendo yasiyoambatana na utamaduni wa watu (Kieti na Peter, 1990; Wanjohi, 1997). Haya hufanyika kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa wazi kwa azma ya kutoa maelekezo yanayohitajika kulingana na tajiriba, mazingira au utamaduni wa watu. Hili linapochipuza, watu huweza kuwa na mitazamo inayofanana (yenye kikoa kimoja) au inayotofautiana (vikoa ambavyo vina tofauti za fasiri). Katika kubainishia maadili katika utamaduni wa jamii, methali huweza kuchukuliwa visivyo kwa mtazamo unaopingana katika uwasilishaji wa ujumbe.

### 2.1 Dhima ya Methali Kinzani katika Ufafanuzi wa Ujumbe

Methali kinzani hufafanua zaidi ujumbe wa kimaadili kwa kuwasilishwa kwa namna mbili: ubainishaji ujumbe moja kwa moja au kwa kutafakari ujumbe wa vinyume vya methali. Kadhalika, methali za Kiswahili huweza kutumiwa katika kuuwasilisha ujumbe wa kijumla katika uelekezaji-rejelezi wa maadili katika jamii kupitia ukinzani unaoleta pamoja mawazo tofautitofauti yanayochangiana. Ubainishaji huo unaweza kufafanuliwa katika viwango viwili: katika methali moja ambapo kuna sehemu mbili kimuundo na pia kupitia ujumbe unaowasilishwa kwenye methali mbili au zaidi (hasa kwa uelekezi wa muktadha wa ujumbe). Kwa kuzingatia Nadharia ya Udenguzi, Derrida (1967) ana maoni kuwa, ishara ambazo hufafanuliwa zaidi kwa kuzingatia maana ya ndani huhitaji tafakari inayoendeleza zaidi maana ya juujuu inayotokana na mkururo wa maneno yanayotumika katika kauli. Hivyo, methali kinzani zinajenga dhana ya uwezekano wa fasiri mbadala. Katika makala haya methali kinzani zinachukuliwa kuwa ni kauli zinazochangia zaidi katika uelewaji wa ujumbe wa kimaadili. Mazingira yanayojengwa katika ukinzani huo ni ya uwajibikaji unaojibainisha kwa sura mbili zinazowiana: usaili na tafakari za kibinafsi na zile zinazohusisha jamii kwa ujumla. Katika makala haya, ukinzani unaozingatiwa ni ule unaopatikana kwenye methali zaidi ya moja ili kudhihirisha namna zinavyowiana katika uwasilishaji wa masuala muhimu ya maadili katika jamii.

### 3.0 Visawe na Ukinzani katika Methali za Kiswahili

Katika methali kuna visawe vya aina mbili: halisi au kamili na vya kiasi. Visawe hivi, aghalabu, hutokana na uzingatiaji maana za maneno yaliyotumika katika ruwaza ya methali mahususi ambayo hugawanyika katika sehemu mbili muhimu: sehemu ya mwanzo inayogusia kiini cha jambo linalohitaji kuzingatiwa na sehemu ya pili ni jibu au matokeo ya sehemu ya mwanzo. Inaweza kuchukuliwa kuwa utaratibu huu ni wa kuhakikisha kuwa kauli kuu huwasilisha hoja au mawazo kwa namna mbili zinazowiana (Kimaro, 2013). Kuwapo kwa uwasilishaji wa mawazo kwa namna mbili kunajikita katika kuondoa viwingu tata vinavyoweza kujitokeza katika upokezi wa ujumbe. Mifano inayoweza kutumika kubainishia hoja katika methali hizi: *'mwenda pole, hajikwai';'pole pole, ndio mwendo'; 'hatua ndefu, hufupisha mwendo'* na *'haraka haraka, haina baraka'*. Methali hizo zinaweza kuwekwa katika kundi moja katika uzingatiaji wa maana ya kijuujuu kuliko maana batini au ya ndani (tazama maneno yaliyopigiwa mstari yanaashiria unyume elekezi wa kiufasiri ambapo methali hizo zina maana hiyohiyo moja). Maneno yaliyopigiwa mstari yanaeleweka kiusambamba, kimetonomia, kiistiara na ukinzani unachangia kueleweka zaidi kwa mawazo yanayowasilishwa.

Methali hizo zinaweza kuwa virutubishi vya kupigia mifano anuwai katika harakati ya ufafanuzi wa ujumbe wa kimaadili ambao unaweza kuwasilishwa moja kwa moja au kwa ubatini wazo. Kutokana na maana za maneno yaliyopo, baadhi ya

watu huweza kuchukulia (kwa haraka) kuwa, methali hizo zinadhihirisha upinzani au ukinzani katika uwasilishaji wa ujumbe sawia. Hivyo, methali hizo zinabainisha mambo mawili: ufinyu na upana wa maana inayotokana na miktadha mahususi ya mawasiliano katika jamii. Kimsingi, methali hujengwa kwa tamathali za usemi (mafumbo) na matokeo yake ni ujumbe kuashiriwa kwa muhtasari au kwa ufupi (Crystal, 1995). Muktadha huu unaweza kujenga mielekeo ya suitafahamu miongoni mwa watu kuhusu methali. Kwa mfano, Faustin Kamugisha katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 24 Januari 2016 kwenye 'Ukumbi wa DINI' (uk. 9) ameeleza kuwa: '… *Kuna ... majina, methali na tamaduni zinazoendeleza uhasama, kulipiza kisasi na kutosamehe. Kuna methali isemayo: "Mavi ya kale hayaachi kunu<u>ka</u>."*

Mwelekeo unaobainika katika unukuzi huo ni wa haraka na unaweza kuchukuliwa kuwa miongoni mwa mitazamo ya kijuujuu ambayo haijajikita katika uanuwai wa miktadha inayoibua matumizi hayo. Kwa mfano, inaweza kuhojiwa kuwa: '… *Methali na tamaduni zinazoendeleza uhasama, kulipiza kisasi na kutosamehe'* zinaeleweka na kubainishwa katika miktadha gani ya kijamii na kuna methali ambayo ina uchanya katika tamaduni za jamii? Hivyo, mwelekeo huo uliochukuliwa ni wa kijumla mno, butu na kavu ambapo kauli iliyotolewa hapo juu inaeleweka katika ufinyu na mitazamo hasi. Isitoshe, mawazo hayo yanaweza kuwa kiwakilishi cha mielekeo hasi ya baadhi ya watu kuhusu fasiri za methali za Kiafrika. Methali katika jamii (na za Kiswahili zikiwamo) zina nguvu na zimekuwa silaha ya kuelekezana na kutokomeza uadui wa ndani kwa ndani katika jamii. Dhima ya methali ni kudumisha ushirikiano, utangamano na amani katika jamii.

Aidha, methali za Kiswahili zinapopigwa darubini, hudhihirisha kiwango fulani cha ukinzani au upinzani katika methali mbili au zaidi. Mifano hapa ni kama: '*mavi ya kale hayanu<u>ki</u>'* na*'mavi ya kale hayaachi kunu<u>ka</u>'*; '*maneno makali <u>hayavunji</u> mfupa'* na *'maneno <u>hukata</u>'*; *'aliye juu mngoje chini'* na '*aliye juu yu juu'*. Methali ya '*mavi ya kale hayanu<u>ki</u>'* inaashiria ukweli unaotokana na tajiriba ya wanajamii. Ukweli huo unakubalika kutokana na maelezo ya mantiki au jambo ambalo limewahi kushuhudiwa (Msokile, 1993). Methali ya *'mavi ya kale hayaachi kunu<u>ka</u>'* inaashiria ukweli wa kiuhusishi ambapo maana inayokusudiwa huweza kubainishwa kupitia muktadha wa kijamii unaorejelewa. Hii ni kwa sababu *'mavi'* hunuka kwa wakati uliopo, muda mfupi au siku chache; baada ya kupigwa upepo kwa muda mfupi au kwa siku kadhaa, uvundo unaokirihisha utakuwa umetoweka kabisa. Katika muktadha huu, neno '*mavi'*, linaweza kuwekwa katika kundi moja lakini fasiri zikawa tofauti. Ujumbe unaowasilishwa kupitia kmethali inayoashiria unyume hupanua zaidi mawazo ya wanaowasiliana. Mawazo yanayopatikana kupitia vinyume vya methali, hayapaswi kupuuzwa katika uelekezaji wa maisha ya watu. Methali hizo zinashadidia ujumbe uanowasilishwa kwa kumfanya anayeshiriki mazungumzo hayo kuwa na maono ya pande mbili (upande unaoeleza na upande unaowasilisha mawazo yanayoashiria kinyume). Kwa mintarafu hii, kuna jozi za methali hizo ambapo moja huwa na ujumbe huu na nyingine kuwa na maana

ile. Jozi nyingine yenye ukinzani kama huo ni: *'haraka haraka, haina baraka'* au '*pole pole, ndio mwendo'* na *'ngoja ngoja, huumiza matumbo* au *adui mpende* na *'akutendaye mtende, mche asiyekutenda'* na *'aliyekuudhi mridhi'*. Mifano hiyo ichukuliwe kuwa ni ukwasi unaopatikana kwenye kauli teule zinazotumika katika mawasiliano ya jamii ambapo kwa kawaida, masuala muhimu hufafanuliwa kwa kudhibitiwa. Uzingatiaji wa pande mbili, uchanya na uhasi, husaidia katika ubainishaji zaidi wa ujumbe unaowasilishwa na wala si hoja zinazopingana, na huu ni ushuhuda katika maisha ya wanadamu. Katika kufanya hivi, jamii huweza kujiopoa kutoka kwenye mitazamo finyu katika kushughulikia masuala muhimu ya kijamii (Ayodi, 2017; Salla, 2014). Hii inamaanisha kuwa, maana inayorejelewa hupata fasiri inayokusudiwa kwa kuzingatia miktadha ya kijamii.

### 3.1 Methali kama Kauli za Mafumbo

Methali ni semi zenye maana fiche zinazokubaliwa na kutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii. Ujumbe katika methali husetiriwa na ni vigumu kueleweka kwa urahisi katika mawasiliano ya watu (Mkota, 2009; Maitaria, 2014). Hivyo, yule anayewasilishiwa huhitaji kujikuna kichwa ili kuweza kuioanisha methali husika na hali halisi katika maisha. Methali huwa kivutio katika sikio la anayekusudiwa ujumbe. Kadhalika, methali huwa vito vya kujengea tafakari kwa kuyapa nguvu masuala muhimu kwa kuzingatia pande mbili zinazohusiana: kibinafsi na ya kikundi cha watu au jumuiya pana (kijumla). Anayekusudiwa katika maongezi, hupanua maarifa katika kuliajiri bongo. Mawazo mbalimbali yanahitaji kufafanuliwa ili kuweza kufanya maamuzi mwafaka. Haya ni mambo ambayo hayawezi kubainishwa kwa kuzingatia kauli moja. Usaili na tafakari zaidi huibuliwa kupitia methali nyingine ambapo maelezo na majibu yenye uzito pia hupatikana huko. Kwa mantiki hii, ujumbe unaowasilishwa kupitia methali hizo unaweza kueleweka kwa ufaafu zaidi kwa kuzingatia miktadha ya kijamii inayorejelewa. Methali ni kauli ambazo zinahitaji umakini ili kuweza kuibua maana iliyokusudiwa na kufasiriwa kwa kurejelea tukio au muktadha mahususi katika jamii. Pasi na kuzingatia miktadha mahususi, kuna hatari ya kudhalilisha na kupuuza dhima ya methali kinzani katika uelezaji wa maadili katika jamii.

### 3.2 Ukariri Mbadala wa Ujumbe Unaowasilishwa

Ingawa methali zinaweza kuainishwa kimakundi, kimaudhui na kimaana; methali hizo hutumiwa katika usisitizaji wa ujumbe kwa kuzingatia unyume au ukinzani wake (Wolfgang na Litovkina, 1999; Salla, 2014). Kwa kutumia methali moja, ujumbe huwasilishwa kwa mkato na maelezo huwa makavu (ya aina moja na ya kijumla mno). Mtazamo huo ni kinyume na ule unaobainika katika ukinzani wa methali zaidi ya moja. Kuna matumizi yasiyo ya pande mbili kama inavyobainika katika baadhi ya methali kinzani. Uzingatiaji wa methali hizo, unanyima uhusishaji wa viashiria vya ujumbe unaotokana na methali zinazowasilisha jumbe za unyume. Methali hizo hufunua pazia kuhusu uanuwai wa mawazo ambayo pia yana

umuhimu katika kuukoleza zaidi ujumbe unaowasilishwa. Katika muktadha huu, uhasi kuhusu methali huweza kujengwa katika akili ya wale wanaoshiriki mazungumzo. Hapa ieleweke kuwa kuna aina mbalimbali za methali zinazoweza kuwa visawe vya maana na zingine kuwa katika upande mwingine japo zinaekeleza dhima hiyohiyo ya kuufafanua zaidi ujumbe unaowasilishwa. Mifano hapa ni: '*subira huvuta heri'; 'ngoja ngoja huumiza matumbo'; 'mvumilia kibivu hula kibovu'*. Methali hizi zimetawaliwa na zimekariri dhana ya 'subira' kwa njia tofautitofauti: manufaa ya watu kutokuwa na papara (Trench, 2003; Kagwa na Waihiga, 2007). Katika jamii, huo ni mwelekeo unaochukuliwa kuwa kielelezo cha utu na maadili katika jamii.

Mwelekeo wa pili ni ule unaoeleza kuhusu hasara ya 'subira', unaoweza kuchukuliwa kuwa ni mtazamo mwingine kuhusu 'subira'. Katika mazungumzo ya kawaida, mwasilishaji anaweza akaanza kwa methali hiyo ya '*subira huvuta heri'* lakini anayeelekezwa ujumbe anaweza kuwa amesinywa na '*ngoja ngoja'* na *'uvumilivu'.* Katika hatua hii mwelekezaji anatarajiwa kufafanua zaidi kuhusu umuhimu wa 'subira' katika maisha kwa kulinganisha na uhasi wake kama unavyoshuhudiwa katika maisha. Katika muktadha huu, mwasilishaji hupata fursa ya kufafanua zaidi (labda kwa mifano) kuhusu uhasi wa kutoandama mwafaka wa 'subira'. Inapotokea hali hii, inabainika kuwa mjadala unaweza kuchochewa kwa kuzingatia methali pinzani na matokeo ni kwamba ujumbe hupata ufafanuzi wa kina. Hapa kuna haja ya kuzingatia ule mwafaka wa mwanzo unaodokezwa kupitia methali chanya ya '*subira huvuta heri'.* Kwa mantiki hii, ni vyema kwa wahakiki kuwa wenye mtazamo mpana katika uchanya na uhasi wa methali, la sivyo, kuna hatari ya kuwa na mtazamo finyu kuhusu uelekezaji mwafaka wa kushughulikia baadhi ya masuala muhimu ya kimaadili katika jamii. Methali nyingine zinazoweza kuzingatiwa ni kama vile '*damu ni nzito kuliko maji'* ambapo ujumbe unaowasilishwa huweza kueleweka kwa uwazi zaidi kupitia kwa *'mtegemea cha nduguye, hufa maskini*' na '*jirani ni bora kuliko ndugu aliye mbali'*. Tazama pia jozi zifuatazo za methali: *'msema kweli ni kipenzi cha Mungu'* na *'ukitaka salama ya duni, funga ulimi wako'* au *'fuata nyuki, ule asali'* na *'fuata nyuki ukafe mzingani'; 'kidole kimoja hakivunji chawa'* au *'mkono mmoja hauchinji ng'ombe,* na *'nahodha wawili chombo huenda mrama'* au *'wapishi wengi huharibu mchuzi'*. Ingawa methali hizi zinaonekana kukinzana, ukweli ni kwamba, zinachangiana katika kuusukuma mbele ujumbe unaowasilishwa. Kwa kuzingatia Nadharia ya Semiotiki, vipengele sita huhusishwa katika mawasiliano muhimu ya watu (Jacobson, 1960). Vipengele hivyo ni: mwasilishaji, mpokezi (hadhira), muktadha, matini, tukio, na msimbo. Kulingana na Lackoff na Johnson (1980), ujumbe muhimu unaowasilishwa kwa hadhira hushirikisha matini teule ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi. Kadhalika, tamathali hizo huweza kuwa za aina mbili: kauli za kitaashira (metonomia) na kauli za kiistiara (kimafumbo). Kauli ya kiistiara (methali ya mwanzo inayotumika) ndiyo ya msingi kwa namna ambavyo inaukoleza ujumbe unaowasilishwa. Methali hiyo hujenga mazingira ya usaili na kuchochea

tafakari kwa hadhira. Kauli za kitaashira (methali nyinginezo) huchangia katika ufafanuzi wa ujumbe katika methali msingi. Kwa hivyo, ni kosa kuchukulia kuwa methali kinzani zinaupotosha au zinaasi mwafaka unaofumbwa katika tamaduni za wenyeji.

### 3.3 Methali kama Kauli Teule za Kujengea Kumbukumbu Isiyosahaulika

Kwa kuzingatia historia ya wenyeji wa Afrika ni kwamba, watu walitegemea zaidi mawasiliano ya ana kwa ana. Jambo hili bado linaendelea hadi wakati wa sasa ambapo asilimia kubwa ya wenyeji wa bara hili inaishi vijijini na mawasiliano ya ana kwa ana ndiyo yanategemewa zaidi katika upashanaji wa masuala muhimu ya kimaadili katika uhalisi wa maisha na ujumla wa tamaduni zao. Hivyo, matumizi ya methali yameshamiri zaidi katika harakati za kuelekezana na kuonyana kuhusu namna watakavyoishi katika misingi ya utamaduni wao. Kwa ambavyo methali ni kauli zinazojirejelea, huwa ni vito vya kubebea busara na hekima ya jamii. Zinapotumiwa kwa mwafaka, hugonga ndipo na nguvu yazo huacha athari kubwa katika akili ya washiriki katika mazungumzo ya kuelekezana. Zaidi ya kwamba methali zimejengeka kwa miundo yenye urari wa sauti na maneno mahususi, huusawiri ujumbe kwa namna isiyosahaulika na mvuto wake hukora sikio la nje na matokeo yake ni kupata hifadhi katika bongo za watu. Mifano inayoweza kuzingatiwa ni takriri ya maneno yaliyopigiwa mistari ambayo yanajenga mahadhi katika methali zifuatazo: *'<u>haraka haraka</u>, haina baraka'* au '*<u>pole pole</u>, ndio mwendo';* na *'<u>ngoja ngoja</u>, huumiza matumbo'*. Kutokana na mahadhi yaliyopo kwenye methali, watu hukumbuka kwa urahisi yale maneno yanayorudiwarudiwa. Urudiaji wa maneno haujengi tu mahadhi au ridhimu katika kauli, pia ni msingi wa kufaulisha ukariri na upokezi wa ujumbe (Parry, 1971; Hawkes, 1979). Kutokana na ukariri huo wa maneno, methali za Kiswahili hutekeleza dhima ya kuelimisha, kutafakarisha na kuhifadhi amali adimu za utamaduni wa jamii. Hapa ieleweke kuwa, methali ni kauli zinazokumbukwa katika jamii kwa namna ambavyo hubeba zaidi ya maana moja na kuvuka vizingiti vya kihisia. Hivyo, sauti zenye mahadhi na ridhimu katika methali huwa kitumbuizo katika sikio la anayeshiriki mazungumzo na matokeo ni kuhakikisha ujumbe unaowasilishwa hupata nafasi maalumu katika kumbukizi zisizokufa katika bongo za watu.

## 4.0 Kauli za Kuzua Mjadala kabla ya Kufikia Maamuzi ya Kuwajibika

Jamii ya sasa imepitia mabadiliko mengi ambapo yanahitaji upekuzi kwa jicho pevu la usaili badala ya mtazamo mmoja wenye masharti. Mwafaka wa kujifunza na kuelekezana unatokana na kustahiana, kupatana, na kuelewana kwa wanaoshiriki mazungumzo. Kinachohitajika hapa ni kushauriana na kuelekezana kwa matarajio ya kujenga mazingira ya kuchochea shauku ya kibinafsi au ya kijamii katika kufikia maamuzi ya kutegemewa. Hapa ieleweke kuwa katika uwasilishaji wa mawazo-tegemewa, kauli za busara hazipingani, vilevile methali hazikinzani bali ni sura mbadala katika kufikia suluhu. Hapa ieleweke kuwa methali kinzani zinaweza kuwa

ni vinyume vya methali. Kwa uelewa huo hapatakuwa na mparaganyo wa mawazo yanayowasilishwa. Sababu hapa ni kuwa, busara huwasilishwa moja kwa moja au kwa kushadidiwa zaidi kwa vinyume vyake visivyokinza ujumbe unaowasilishwa.

Mawazo yanayothaminiwa katika jamii hayatarajiwi kupatikana kwa urahisi ila kwa 'usasanyaji wa usanishaji wa mawazo.' Hapa tafakari za aina mbili zinabainika: inayozingatia taratibu (polepole, subira, makini) na ile inayoingatia haraka (pupa). Mifano ya methali hizo ni kama: *'damu ni nzito kuliko maji'* au *'mtu hachagui ndugu'* na *'mtegemea cha nduguye hufa maskini'* na *'heri jirani aliye karibu kuliko ndugu aliye mbali'*. Methali hizo zinaweza kutofautiana kwa kuzingatia maana inayotokana na maneno yaliyotumika lakini inakuwa msingi wa kuelekezea na kuchochea mjadala wa kitafakuri ambapo inabainika kuwa *'ndugu'* ni muhimu kwa kuwa wana unasaba. Hata hivyo, hiyo si hoja kwa kuzingatia mantiki ya methali kinzani; kwa sababu *'jirani'* anaweza kutoa msaada wa dharura unapohitajika. Wazo hilo linaweza pia kupigiwa mfano kupitia methali ya *'fimbo ya mbali, haiui nyoka'*. Kutegemea aina, mwelekeo, na uzito wa maadili yanayowasilishwa, tafakuri inayostahili inaweza kupatikana katika ukinzani wa methali moja lakini tafakari zaidi hujengwa katika matumizi ya ukinzani wa methali mbili au zaidi. Ni katika muktadha huu ambapo methali huchukuliwa kuwa kurunzi ya kumulikia njia ya kupitia katika maisha isiyokuwa wima. Hivyo, kauli au vito vya hekima hunukuliwa au hurejelewa zaidi katika maongezi muhimu ya watu. Athari ya matumizi hayo ni kujenga mazingira ya usaili zaidi unaohitaji utafiti wa kibinafsi au kimakundi. Hii ni mihimili inayojenga mahusiano ya uungwana na uaminifu yanayojengwa kwenye mazingira ya usemezano wa kurekebishana katika jamii. Hapa ieleweke kuwa, matumizi ya methali hutokana na kuwapo kwa haja inayohitaji ubainishaji na suluhu katika masuala ya kijamii na baadaye (kama hatua ya mwisho) kuwa na njia ifaayo ya kuelekezana katika jamii. Methali hizo zinawiana na kuchangiana katika uwasilishaji wa mawazo. Katika muktadha huu, methali hizo zinasisitiza na zinavuta umakini katika upokezi wa ujumbe unaowasilishwa. Isitoshe, kila mwanajamii huwa mbioni kutaka kuvikwa koja la hadhi na kutambuliwa kwa kutuzwa kutokana na mienendo au taratibu zinazokubaliwa. Hayo ni mambo muhimu yanayokazaniwa siyo tu na vijana bali pia na wazee ambao wanachukuliwa kuwa ni wenye hekima na busara katika jamii.

### 4.1 Njia ya Kudhihirisha Ukomavu katika Uwasilishaji wa Kimaadili katika Jamii

Kwa kuwa methali ni kauli zisizokuwa na maana ya moja kwa moja; zinahitaji umakini unaotokana na subira katika uwasilishaji wa hoja. Hivyo, hazihitaji papara katika ufafanuzi wa maana batini inayokusudiwa. Kwa wale ambao ni wachanga au hawajakomaa kimawazo kama vile watoto na vijana, huweza kuwasilishiwa ujumbe wa kuadilisha kwa lugha ya moja kwa moja. Hili huweza kutendeka kwa kuzingatia miundo katika ukinzani-sahili unaoshuhudiwa kwenye methali moja. Zaidi ya

kunogesha mazungumzo, matumizi hayo ya methali huwa kitambulisho au ithibati ya kutambua mielekeo ya watu wanaoshiriki mazungumzo. Mawazo muhimu ya kimaadili katika jamii huwasilishwa kwa kuzingatia taratibu ambazo huwa fomula katika kuyapa nguvu mazungumzo.

Uzingatiaji wa methali kinzani usichukuliwe kuwa ni njia ya kuparaganya mawazo bali huwa silaha muhimu zinazotumiwa kuratibu hoja kiawamu. Katika hatua ya mwanzo, methali inaweza kutumiwa katika kuibulia mawazo ya kijumla na kubainisha taswira chanya katika harakati ya kujengea dibaji. Kwa mfano, methali *'aliye juu mngoje chini'* inaweza kutumiwa. Methali hii inawataka watu kuwa wenye kuandama subira katika maisha. Katika kuzingatia mawazo yanayowasilishwa ni kwamba, hakuna haja ya kuwa na papara katika kupata suluhu. Methali hii ni sawa na ile ya *'Mgaagaa na upwa hali wali mkavu'*. Baadaye mawazo hayohayo yanaweza kuwasilishwa kwa kuzingatia mwelekeo mwingine kwamba,*'aliye juu yu juu'* hasa inapobainika kuwa aliyeukwea mti amebaki kulekule juu. Hivyo, inawabidi watu kuweza kutumia njia nyingine ya kumfikia yule aliye juu. Hii ni wakati inapobainika kuwa hakuna jingine linaloweza kutumiwa la sivyo itakuwa kupoteza wakati. Kwa njia hii, mawazo huwa yanawasilishwa kihatua na pia kutegemea namna ujumbe huo ulivyopokelewa na wakusudiwa. Hapa ujumbe huwekwa kwenye mizani kwa uelewa ni hoja gani italetwa mwanzo na ipi itakayofuatia na matokeo ni kuwa, ujumbe huwasilishwa kwa mantiki. Isitoshe, matumizi ya methali kinzani katika kubainisha mawazo, husaidia kuiweka kitako hadhira na hutumika kama njia mojawapo ya kubaini ulumbi na ufundi katika uwasilishaji wa ujumbe huo wa kimaadili. Kwa hivyo, inakuwa mtindo katika uzungumzi katika harakati ya uwasilishaji wa ujumbe sawia kupitia namna tofauti. Methali kinzani, ambazo kwa kawaida ni mtazamo wenye pande mbili, zaidi ya kuwasilisha kiini cha mawazo kwa mitindo mbalimbali, pia hubainisha falsafa ya wenyeji wa Afrika kwamba maisha si ya aina moja; kwa hiyo, huweza kuwasilishwa kwa kuzingatia maelezo mbalimbali yanayoafikiana. Hapa inamaanisha kwamba mawazo ya aina moja yanaweza kuwasilishwa kwa njia tofautitofati na kwa maneno tofautitofauti kama njia ya kuufafanua zaidi ujumbe mkuu. Methali zingine zinazoweza kuzingatiwa ni '*usiache mbachao kwa msala upitao'* na *'usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha'.* Hapa ieleweke kuwa mawazo muhimu katika jamii za Waafrika hujikita katika tamaduni zao na methali zitumikazo katika mawasiliano ya ana kwa ana huwa vipopo vya kubeba, kuhifadhi na kuziwasilisha fikra hizo zinazojikita katika tamaduni za watu.

**4.2 Ukwepaji wa Mielekeo ya Kihisia na Mihemko**

Katika jamii za Kiafrika aghalabu masuala ya muhimu huwasilishwa kwa kauli mshindo zenye nguvu na ukemeaji unaostahili; hakuna kubembelezana katika juhudi za uelekezaji na urekebishaji au 'ulainishaji' wa mtu kukubalika na watu. Ujumbe unaohusu maadili huwa kwa manufaa ya umma kwa jumla. Kwa kukaidi

uelekezi unaotarajiwa katika misingi ya utamaduni wa jamii; adhabu stahiki zipo kama nembo na zimebainishwa. Mifano hapa ni: *'akutendaye mtende mche asiyekutenda'; 'dawa ya moto ni moto'*. Kwa misingi hii, methali ni kauli ambazo zimejengeka katika mazingira ya uhalisi wa maisha ya watu. Kijuujuu, baadhi ya methali mbili au zaidi zinaweza kuwa na maana mbalimbali ambazo haziupotoshi ukweli wa msingi katika jamii. Mifano ni: '*adui mpende'* na *'Ibilisi ya mtu ni mtu'*. Swali hapa ni: inawezekana vipi kwa mtu ampende adui ilhali anafahamu kuwa mtu huyo ni mbaya? Mjadala unaweza kuzuka lakini kutokana na matumizi ya methali mbili au zaidi; suluhu huweza kupatikana. Hivyo, methali kinzani zinajenga taswira zinazoonekana au za kimawazo ambapo kuna uhitaji wa maelezo ya kina. Kwa kuzingatia mwelekeo huu, watu huweza kufanya uteuzi unaofaa. Endapo mada inayorejelewa itakuwa yenye athari mbaya kwa jamii, kauli ya ukemeaji inaweza kutumiwa kwa methali mbadala. Methali hizo mbadala za ukemeaji ni zile zinazojibainisha kama kinzani. Hapa ibainike kuwa hakuna ukinzani katika matumizi ya methali bali katika harakati ya usisitizaji wa wazo katika misingi ya uhalisi wa maisha.

## 4.3 Methali kama Chombo cha Mawazo Endelevu katika Jamii

Kimsingi, mawazo huwa hai na kila uchao huwa yanabadilika. Kauli teule huwapo ili ziwatumikie na wala si kuwa wafungwa wa kauli hizo. Huwapa wapokezi wa ujumbe, kushiriki kikamilifu katika mazungumzo (Wolfgang na Litovkina, 1999; Trench, 2003). Hivyo, methali ni kauli zilizo hai; hutumiwa kwa matarajio kwamba maana ya ndani (iliyosetiri ujumbe) itapatanishwa na yale yaliyopo katika jamii. Isitoshe, methali ni dira elekezi ya kumwongoza mtu kuwa mtu miongoni mwa wenziwe katika jamii (Wanjohi, 1997). Kwa maana hii, methali ni jukwaa la kujengea na kukuzia stadi za wasikilizaji kwa upande wa kuongea na kusikiliza. Kwa mfano, pale ambapo ujumbe haujaeleweka hadhira ina hiari ya kusemezana na mwasilishaji ambapo hana budi kutoa ufafanuzi kwa kushirikisha mifano kadha wa kadha ili kushadidia hoja ya kimaadili inayorejelewa. Methali zinapotumiwa kuna matarajio mawili au matatu ambayo yanahitaji kuelezwa: usemezano, utoaji wa ufafanuzi na ushadidiaji wa hoja zinazowasilishwa. Kadhalika, katika mazungumzo yanayogusia masuala ya kuelekezana kuhusu maadili katika jamii, huwapo pande mbili: mwelekezaji na mwelekezwaji ambapo kila upande una muda wake wa kutulia ili kusikiliza kwa kuheshimiana. Katika hayo yanayoelezwa, mojawapo ndilo linalopaswa kuzingatiwa na mengine huwa yanajenga uziada unaoshadidia tu.

## 4.4 Methali Kinzani kama Kauli Husishi

Matumizi ya methali kinzani yanahitaji kuhusishwa na yale yanayopatikana katika tajiriba ya watu. Aghalabu, wanaotumia mifano ya methali hizi huchukuliwa kuwa wamepitia mengi katika maisha yao. Aidha, kwa wale ambao bado hawana tajiriba pana kuhusu maisha, wanachukua tahadhari ya kuepuka dhiki au vishawishi vinavyoweza kuwafanya waonekane wakiukaji wa utamaduni wa jamii. Kadhalika,

methali inaweza kueleweka kwa kuzingatia miktadha ya kijamii. Maana kusudiwa haiwezi kueleweka kwa kuzingatia maneno yaliyotumika bali maneno hayo ni viashiria vya yale yanayopatikana katika utamaduni wa jamii. Katika muktadha hu-u, methali zinazoonekana kukinzana zinashirikiana katika ujumbe unaowasilishwa.

## 5.0 Uanishaji wa Mawazo kwa Kuzingatia Methali Kinzani

Katika kuzingatia kipengele cha ukinzani, methali za Kiswahili zinaweza kuainishwa kwa kuhusisha baadhi ya mambo yafuatayo: uzito wa ujumbe unaowasilishwa, idadi ya methali zinazotumika katika uwasilishaji ujumbe, kiwango cha tafakuri cha hadhira na aina ya ujumbe unaowasilishwa. Methali zinazokemea na zinazosuta huweza kuwa kauli za moja kwa moja au mawazo hayo yanaweza kuwasilishwa kupitia methali kinzani. Mifano hiyo ni: *'asiyesikia la mkuu huvunjika guu'; 'mwiba uchomeapo ndiko utokeapo'; 'nyani haoni kundule'.* Hizi ni methali zinazobainisha ukweli wa moja kwa moja unaoweza kuthibitishwa kwa kuzingatia tajiriba ya watu. Methali zinazobainisha ukweli unaotokana na tajiriba ya watu ni: *'asiyekuwepo na lake halipo'; 'mtaka cha mvunguni sharti ainame'; 'mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe'; 'usipoziba ufa utajenga ukuta'*. Zile za kimafumbo ambapo zinaeleweka zaidi katika muktadha wa utamaduni maalumu wa jamii (mifano ni: *'mgaa na upwa hali wali mkavu'; 'Mgalla muue na haki yake uumpe'; 'mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani'*. Kadhalika, kuna zile zinazotokana na athari au mabadiliko ya tamaduni kutoka nje ya jamii (Mifano ni: *'baniani mbaya kiatu chake dawa'; 'Hindi ndiko kwenye nguo na wendao uchi wako'; 'ukistaajabu ya Mussa, utayaona ya Firauni'; 'Mtoto mkadi hafaidi hadi siku ya idi'*).

## 6.0 Hitimisho

Methali kinzani za Kiswahili hutekeleza dhima muhimu katika mazungumzo ya wanajamii. Aghalabu, ujumbe wake huwasilishwa kwa azma ya uelezaji na uelekezaji. Aidha, maelekezo hayo huzingatia mitindo isiyo ya moja kwa moja. Ili fasili mwafaka kuweza kuafikiwa, kuna haja ya kuhusisha ujumbe unaotokana na methali hizo na yale yanayotokana na tajiriba za wenyeji. Uelekezaji wa maadili katika jamii hujengwa kwa namna mbili: kwa kupitia tafakari - unaolenga kufikia uamuzi binafsi au ule unaoshurutishwa. Aidha, methali kinzani hutoa mwelekeo wa kuelekezana unaoimarisha zaidi mahusiano ya wanajamii. Katika makala haya, imebainika kwamba, methali moja inaweza kuwa na ukinzani wa wazi (ambapo hili, si tatizo) kwa kuwa tayari watu wanafahamu kimazoea. Mtazamo huo ni 'ndani kwa ndani' na umezowewa katika mawasiliano ya jamii. Fasili finyu au ya kijumla inaweza kurejelewa kwenye mtazamao huo. Methali kinzani au vinyume vya methali ni msingi wa uelezaji na uelekezaji wa maadili katika jamii. Kadhalika, methali hizo zinaweza kutumika kuelekeza kuhusu masuala tata na pia kuwa ni njia ya kujenga mazingira ya usemezano unaolenga usuluhishaji wa matatizo ya maisha ya watu katika jamii.

## Marejeleo


Adungo, C. (2015) "Ujumuishaji na uchukulio katika sentensi" katika *Taifa Leo, tarehe* 2 Februari 2015. uk. 20.

Ayodi, N.K. (2017) "Tafsiri na Fasiri ya Methali za Kimaragoli: Hazina katika Fasihi ya Kiafrika". Katika M. Kandagor (Mh.) *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Eldoret: Moi University Press. kur. 327-334.

Crystal, D. (1995) *The Cambridge Encyclopedia of the English Language.* London: Cambridge University Press.

Derrida, J. (1967) *Jacquies Derrida of Grammatology.* London: John Hopkins University Press.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa.* London: Oxford University Press.

Gesero, W.C. (2009) *Methali za Kiswahili Afrika Mashariki na Kati*. Dar es Salaam: ABSITCO.

Hawkes, T (1979) *The Structuralism and Semiotics*. London. Methuen.

Jacobson, J.W. (1960) "Concluding Statement: Linguistics and Poetics". Katika J. Seboek (Mh.) *Style and Language.* Cambridge: MIT. kur. 171-185.

Kagwa, F.M. na Waihiga, G. (2007) *Kamusi Changanuzi ya Methali.* Nairobi: Mcmillan Kenya Ltd.

Kamugisha, F. (2016) "Msitari kati ya Wema na Ubaya ni Mwembamba". *Taifa Leo.* 24 Januari 2016. uk. 9.

Kimaro, H. (2013) "Dhima ya Fasihi Simuliz katika Jamii". *Taifa Leo*. 31 Novemba 2013. uk. 24.

Kieti, M. na Peter, M. (1990) *Barking, You'll Be Eaten! The Wisdom of Kamba Oral Literature*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Kimaro, H. (2013) "Dhima ya Fasihi Simuliz katika Jamii." *Taifa Leo*. 31 Novemba 2013 kwenye safu ya 'Lugha na Fasihi' (uk. 24).

Lakoff, G & Johnson, M. (1980) *Metaphors We Live By*. Chicago: Chicago University Press.

Madumulla, J.S. (1995) *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKI.

Maitaria, J.N. (2014) "Dhima ya Methali za Kiswahili kama Chombo cha Kusuluhishia Migogoro katika Jamii". Katika I. Simala; L.C. Mwita, na M. Osore (Wah.) *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications. kur. 133-149.

Maitaria, J.N. (2018) "Utafiti katika Methali za Kiswahili". Katika M. Kandagor (Mh.). *Fasihi ya Kiswahili na Maendeleo yake.* Dar es Salaam: TATAKI. kur. 121-142.

Maitaria, J.N. (2019) "Utata katika Methali za Kiswahili". Katika J. Kobia, M. Kandagor, L.C. Mwita, J.N. Maitaria na Wandera, S. (Wah.) *Lugha na Fasihi katika Uwiano Barani Afrika.* Eldoret: Moi University Press. kur. 163-172.

Mkota, A. (2009) *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi.* Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Mlacha, S.A.K. (1985) "Dhima ya Methali katika Malezi". *Kiswahili,* Juz. 52/1 na 52/2 1985:175-186.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Publishers Ltd.

Nsookwa, J. (2011) "Dokezo za Methali za Ishara katika Methali za Kiganda." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala.

Nyariki, E. (2014) "Chimbuko la Baadhi ya Methali na Misemo'. *Taifa Leo.* 20 Julai 2014.

Parry, A. (1971) *The Making of the Homeric Verse: The Collected Papers of Milman Parry*. Oxford: Clarendon.

Salla, H.D. (2014) *Methali za Kikwetu.* Dar es Salaam: Africa Proper Education Network.

Schlee, G. na Sahado, K. (2002) *Rendille Proverbs in their Social and Legal Context.* Köhn: Rüdiger Köpper Verlag.

Trench, R.C. (2003) *Proverbs and Their Lessons*. London: George Reutledge and Sons Ltd.

Wafula, R.M. (1994) "Uainisho wa Methali". *Writers Forum Journal of the Writes' Association of Kenya,* Juz 2A: 63-68.

Wanjohi, G.J. (1997) *The Wisdom and Philosophy of Gikuyu Proverbs: The Kihooto Word - View.* Nairobi: Paulche Publications Africa.

Wolfgang, M. & Litovkina, A. (1999) *Twisted Wisdom: Modern Anti-Proverbs.* Burlington, VT: The University of Vermont.